JINA……..……NAMBA YAKO……..… TAREHE……..

SHULE……..…… SAHIHI YA MTAHINIWA……..…

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya Pili
LUGHA
Saa: 2 ½

TATHMINI YA PAMOJA KCSE
WILAYA ZA KISUMU KASKAZINI NA MASHARIKI
JULAI / AGOSTI 2010

MAAGIZO

- *Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- *Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
- *Jibu maswali **yote.***
- *Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- *Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

KWA MTAHINI PEKEE

SWALI	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Karatasi hii ina kurasa kumi zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa

UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

UBAGUZI

Mtu yeyote atakayejishughulisha na uhusiano kati ya watu atagundua kwamba uhusiano kati ya watu wa makabila au mataifa mbalimbali msingi wake hautokani na kuwako na rangi moja au utamaduni sawa tu kati yao bali na sababu zingine nyingi pia.

Kuna sababu kubwa tatu zinazowagawanya watu wengi duniani. Sababu zenyewe ni tofauti za rangi, tofauti za kitamaduni na tofauti za kiuchumi. Pia tunaweza kuongeza sababu ya nne-ubaguzi wanaofanyiwa wanawake katika nchi nyingi. Hii ni sababu kubwa ya nne inayogawanya jamii na kuzuia ushirika kamili.

Yajulikana wazi kuwa huku kwetu zama za ukoloni kulikuwa na ubaguzi wa rangi. Watu walilazimishwa kuishi, kufanya kazi, kwenda skuli, kutangamana na hata kuabudu na watu wa rangi yao pekee. Matokeo yake ni kuwa kukawa na mgawanyiko wa shughuli za kisiasa na za kiuchumi na jambo hilo likazusha watu wa rangi mbalimbali kulinda kwa nguvu kubwa mali na haki zao. Ingawa mtindo huu wa ubaguzi sasa umevunjiliwa mbali bado masalia ya utengano na kutoaminiana na hata kuchukiana kati ya watu wa rangi mbalimbali kumebaki.

Tuzungumzapo juu ya utamaduni tunafikiria tabia, mila na desturi tulizokuwa nazo toka tungali watoto. Tofauti za utamaduni kati ya makabila mbalimbali ndizo zinazoleta kutoelewana kwa vile kila kabila laona kuwa utamaduni wake ni bora kuliko wa makabila mengine.

Tofauti zinazoletwa na hali ya uchumi je? Watu wenye hali nzuri ya kiuchumi aghalabu hujiona ni bora kuliko wale wa hali ya chini. Hii ni fikira ya hivi karibuni tu kwani katika maisha ya kimila ya kiafrika hapo zamani utajiri wa mtu haukumfanya ajione bora au awe na mamlaka juu ya wenzake. Juu ya hayo watu wote waliangaliwa na kushiriki katika kila shughuli pamoja na kwa faida ya kila mtu.

Sasa tuangalie jambo la mwisho, yaani kubaguliwa kwa wanawake. Swala hili la ubaguzi kwa wanawake ni tatizo la ulimwengu mzima na huzuka takribani katika kila kabila au taifa.

Tukipeleleza tutaona kuwa katika makabila mengi,wanawake wako katika hali ya chini. Mfano mmoja pengine utadhihirisha hali hii vyema. Uchunguzi umehakikisha kwamba ukiangalia idadi ya wakulima katika baadhi ya nchi za kiafrika utaona kuwa kuna wanawake wengi kuliko wanaume lakini wanawake hawana usemi au mamlaka

yoyote katika kuendesha uchumi wa kilimo; wanaofaidi ni wenye mashamba ambao wengi wao ni wanaume.

Basi tunaweza kusema kuwa maendeleo katika nchi yoyote hayatakuwa yakipatikana ikiwa watu wake watakuwa wakibaguana kwa ajili ya rangi, utamaduni, hali ya uchumi na hali ya maumbile yao yaani kwa kuwa ni wanawake au wanaume.

MASWALI.

a) Eleza msingi wa ubaguzi duniani. (alama 4)

……

……

……

……

b) Utamaduni, kulingana na taarifa hii, una maana gani? (alama 2)

……

……

……

……

c) Hivi leo katika mataifa mengi, ubaguzi hutokana na hali ya kiuchumi kwa kiwango kikubwa. Fafanua. (alama 2)

……

……

……

d)Kwa maoni yako, eleza sababu za mwanamke kubaguliwa hasa katika jamii nyingi za kiafrika. (alama 3)

……

……

……

……

e) Eleza athari ya ubaguzi katika nchi za kiafrika. (alama 2)

……

……

……

……

f) Toa maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika taarifa. (alama 2)

(i)Ubaguzi ……

……

(ii)Masalia ……

……

UFUPISHO

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali.

Kuna wataalamu siku hizi wanaosema kuwa jela si pahala pa adhabu bali pa matibabu. Yaani madhumuni ya kumtia mhalifu jela isiwe kumwadhibu kwa makosa aliyofanya bali iwe kumtibu na kujaribu kumrekebisha tabia yake ili awe raia mwema.

Zamani wahalifu waliadhibiwa kwa mujibu wa makosa waliyoyafanya. Mhalifu aliyefanya makosa madogo madogo alifungwa lakini mtu aliyeua naye aliuawa.

Sasa wataalamu wanatuambia kuwa mhalifu akiadhibiwa anapokuwa kifungoni, basi akitoka hurejea tena kufanya uhalifu. Madhumuni ya kumtia jela iwe si kumwadhibu bali kumfunza tabia njema. Wanatuambia kuwa makosa afanyayo mhalifu yanatokana na matatizo ya jamii kwa jumla, nayo ni matatizo kama ya umaskini, msongamano wa watu katika miji, ugomvi manyumbani baina ya wazazi na kadhalika. Kwa hivyo, kwa mujibu wa wataalamu hawa, kosa afanyalo mhalifu si kosa lake pekee bali ni kosa la jamii nzima

Jitu lililozoea kuua halioni kitu kumpiga kisu mwanamke njiani au kumpiga mtarimbo au rungu la kichwa na kumyang'anya kila alicho nacho. Siku hizi, jitu kama hili baadhi ya wataalamu husema lisiuawe, lifungwe maisha tu. Lakini 'kifungo cha maisha' ni kama tunavyokijua. Muuaji hufungwa pengine miaka kumi tu kisha husamehewa muda uliobaki. Hapo tena huwa huru ama kuifichua mali aliyoiiba na kuistarehea raha mustarehe au kurejea tena kufanya uhalifu.

Haya ni kinyume kabisa na mambo yaliyokuwa zamani. Aliyeua aliuawa kwa hivyo watu waliogopa kuua. Raia na pia askari waliokuwa wakiwasaka wahalifu walinusurika vifo kwani wahalifu wengine walichukua silaha za hatari kama bastola na bunduki.

Sasa wale wahalifu wabaya sana-mijizi, minyang'anyi na wauaji-ndio wanaotukuzwa. Magazeti huwashawishi makatili hawa na kuwapa mapesa chungu nzima waeleze maisha yao ya kikatili. Magazeti haya sasa ndiyo yanayopata wasomaji wengi. Pia wachapishaji vitabu vya hadithi zinazohusika na uhalifu, biashara zao

zinazidi kustawi. Kadhalika sinema zinazoonyesha picha za ukatili; wizi na mauaji hujaa watazamaji wanaoshangilia uhalifu ufanywao.

Wahalifu kwa upande mmoja wanatukuzwa na masinema, vitabu na magazeti na kwa upande mwingine "haki" zao zinapiganiwa na baadhi ya wataalamu. Watu wanaowalaani wahalifu ni wale waliohasirika tu na kuteswa na wahalifu. Baadhi yao hata kulaani hawawezi kwa sababu wameshauawa, hawana tena kauli.

MASWALI

a) Chagua anwani mwafaka kwa taarifa hii. (Maneno yasizidi manne) (alama 1)

……

……

b) Eleza mtazamo wa baadhi ya wataalamu wa sasa kuhusu adhabu kwa mhalifu. (Baina ya maneno 25 na 30) (alama 8)

Matayarisho

……

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

c) Anayeua asiuawe,afungwe kifungo cha maisha tu. Mwandishi wa hii taarifa anapinga hayo. Toa sababu zake. (Maneno 25) (alama 6)

Matayarisho

……

……

……

……

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

MATUMIZI YA LUGHA

a) Nomino hizi ni za aina gani?

(i) Mafuta……

(ii) Kusoma……..

(alama 2)

b) Andika upya sentensi zifuatazo kwa kufuata maagizo.

(i) Usipotia bidii, hutafaulu. (yakinisha) (alama 2)

……

……

(ii) Mama aliketi babu alipoondoka. (Andika kinyume.) (alama 2)

……

……

(iii) Utamuarifu ukimwona. (Kanusha) (alama 2)

……

……

c) Tambua aina za vielezi katika sentensi hii.

Mara kwa mara yeye huniongelesha kijinga lakini ninaapa kuwa nikitoka Nairobi keshokutwa, atashangaa nikimnyanyua hobelahobela kwa mikono yangu.

(alama 6)

……

……

……

……

……

……

……

d) Tunga sentensi zozote **nne** kuonyesha matumizi yoyote manne ya kiambishi "KI"

(alama 4)

……

……

……

……

……

e)Tumia kielelezo cha matawi kuchanganua sentensi ifuatayo.

Yeye ni mchezaji hodari. (alama 4)

……

……

……

……

……

……

……

f) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi.

Mwanasiasa mmoja aliwaambia kuwa wasipozinduka na kutetea haki zao ipasavyo, wangeendelea kudhulumiwa katika nchi yao. (alama 3)

……

……

……

……

g) Eleza maana ya: (alama 4)

(i)Mofimu

……

……

(ii)Kiambishi

……

……

(iii)Shadda

……

……

(iv)Kiimbo

……

……

h) Sahihisha sentensi hii kwa ukamilifu.

Ng'ombe ambaye yenye ilinunuliwa imekufa (alama 2)

……

……

i) Kamilisha jedwali kwa mnyambuliko unaofaa. (alama 2)

Kitenzi	Tendewa	Tendesha	Tendeka
Adhibu	……	……	Adhibika
Cha	……	chisha	……

j) Tambua aina za maneno. (alama 3)

(i) Lahaula!……..

(ii) Sembuse……

(iii) Mimi……..

(iv) Nyeupe……..

(v) Yu……..

(vi) Walibora……..

k) Bainisha aina za shamirisho. (alama 3)

Wazazi wengi wamewalipia watoto karo kwa cheki.

……

……

……

……

……

l) Andika katika ukubwa. (alama 1)

Maimuna alimwona mnyama mwenye vichwa viwili.

……

……

……

ISIMU JAMII

Jadili matatizo yanayokumba maendeleo ya Kiswahili nchini na namna ambavyo matatizo hayo yanaweza kutatuliwa. (alama 10)

……

……

……